## 1.0 Utangulizi

Taarifa hii inaelezea hali halisi ya makusanyo ya Halmashauri kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai - Desemba) kwa mwaka wa fedha 2018/19, kwa kuainisha makisio ya mwaka na mapato halisi ya kila Halmashauri, ufanisi wa ukusanyaji na wingi wa mapato hayo kwa kulinganisha na mapato yaliyokusanywa katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2017. Ulinganifu huu umelenga kuonesha jinsi kazi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa inavyoendelea kusimamiwa vyema. Aidha, katika kipindi hicho kuna baadhi ya Halmashauri zimefanya vizuri na zingine zimefanya vibaya.

## 2.0 Uchambuzi

Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri katika taarifa hii umelenga kuonyesha ufanisi wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwa kulinganisha Halmashauri moja moja, makundi ya Halmashauri na Kimkoa. Aidha, taarifa inaonyesha tofauti ya kipindi hiki na kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2017/18.

### 2.1 Mapato ya Halmashauri kwa kuzingatia Asilimia ya Makusanyo

Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Halmashauri zilipangiwa kukusanya **shilingi bilioni 735.6 k**utoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2018 Halmashauri zimekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 300** sawa na **asilimia 41** ya makisio. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri zilipanga kukusanya **shilingi bilioni 687.3** ambapo hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2017, zilikuwa zimekusanya **shilingi bilioni 281.3** sawa na **asilimia 41** ya makisio. Takwimu hizo zinabainisha kuwa, kuna

ongezeko la **shilingi bilioni 18.7** kwa mwaka wa Fedha 2018/19 ikilinganishwa na makusanyo kwa kipindi kama hiki kwa mwaka wa Fedha 2017/18. Uchambuzi huu unaonesha kuwa ni **Halmashauri 33** tu kati ya Halmashauri 185 zimeweza kukusanya Mapato ya ndani kwa kiwango cha **asilimia 50 na zaidi** ya makisio ya mwaka. Aidha, **Halmashauri Ishirini na moja (21)** zimefanya vibaya kwani zimekusanya chini ya **asilimia ishirini (20%)** ya makisio yake ya mwaka. Halmashauri hizo ni; **Halmashauri za Miji nne(4)** na **Halmashauri za Wilaya kumi na saba (17)** ambapo Halmashauri ya mwisho kabisa ni Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu ambayo imekusanya sawa na **asilimia sita (6%)** ya makisio ya mwaka. Kati ya Halmashauri 33 zilizokusanya aslimia 50 na zaidi, **Halmashauri za Majiji ni tatu (3)** zikiongozwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma; **Halmashauri** za **Manispaa ni Mbili (2)** zikiongozwa na Manispaa ya Ilala**,** **Halmashauri za Miji nane (8)** zikiongozwa na Mji wa Geita na **Halmashauri** za **Wilaya ishirini (20)** zikiongozwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Geita** *(Jedwali Na. 1)*

## 2.2 Mapato ya Ndani kwa Mpangilio wa Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya

Uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya Majiji 6, Halmashuri ya Jiji la Dodoma linaongoza kwa kukusanya **asilimia 59** ya makisio. Jiji la Tanga limekuwa la mwisho kwa kukusanya **asilimia 33** ya makisio.

Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imeongoza katika kundi la Manispaa kwa kukusanya ailimia 64 ya makisio ambapo Manispaa ya Lindi imekuwa ya mwisho katika kundi hili kwa kukusanya **asilimia 20** ya makisio.

Kwa upande wa Halmashauri za Miji, Halmashauri ya Mji wa Geita imeongoza kwa kukusanya **asilimia 84** ya makisio na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba imekuwa ya mwisho katika kundi hili kwa kukusanya **asilimia 9** tu ya makisio.

Aidha, katika kundi la Halmashauri za Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imeongoza kwa kukusanya **asilimia 78** ya

makisio ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imekuwa ya mwisho kwa kukusanya **asilimia 6 tu** ya makisio *(Jedwali Na. 2)*

## 2.3 Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa kuzingatia Wingi wa Makusanyo

Halmashauri iliyoongoza kwa kukusanya Mapato ya Ndani kwa wingi ni Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambapo katika kipindi cha Julai – Desemba, 2018 imekusanya **Shilingi Bilioni 40.12.** Halmashauri iliyokusanya kiasi kidogo cha Mapato ya Ndani ni Halmashauri ya Wilaya ya Momba iliyokusanya **Shilingi Milioni 105.04.** Aidha,Halmashauri 64 zimeweza kukusanya zaidi ya Shilingi Bilioni Moja katika kipindi hicho *(Jedwali Na. 3)*.

## 2.4 Mapato ya Ndani ya Halmashauri Kimkoa kwa kuzingatia Wingi wa Mapato

Mkoa ambao umeweza kuongoza katika kukusanya mapato ya ndani katika kipindi cha nusu ya mwaka wa fedha 2018/19 kwa kuzingatia wingi wa mapato ni Mkoa wa Dar es Salaam ambao umekusanya **Shilingi bilioni 77.04** ukifuatiwa na Mkoa wa Dodoma ambao umekusanya **Shilingi bilioni 44.8.** Mkoa wa mwisho katika wingi wa ukusanyaji wa mapato ni Katavi ambao umekusanya **Shilingi bilioni 2.4** *(Jedwali Na. 4).*

## 2.5 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Kimkoa kwa kuzingatia Asilimia ya Makusanyo

Mkoa wa Geita umeibuka kinara kwa ufanisi wa ukusanyaji wa Mapato ya ndani kwa kipindi cha nusu mwaka kwa kukusanya **asilimia 56.4** ya makisio ya mwaka wa Fedha 2018/19 ukifuatiwa kwa karibu na Mkoa wa Dodoma uliokusanya **asilimia 55.9** ya makisio yake. Mkoa wa mwisho kwa kigezo hicho ni Mkoa wa Mtwara ambao umekusanya **asilimia 15** ya makisio yake ya mwaka *(Jedwali Na. 5).*

# 3.0 Halmashauri zilizofanya vibaya nusu mwaka 2017/18

Katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri 10 hazikufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato kwani zilikusanya chini ya asilimia kumi (10%) ya makisio yake. Wakurugenzi wa Halmashauri hizo pamoja na kutakiwa kujieleza walipewa muda wa kujitathmini na kuhakikisha wanaongeza bidii katika suala la ukusanyaji wa mapato. Halmashauri 9 kati ya 10 zilizofanya vibaya zimefanikiwa kufanya vizuri katika nusu mwaka wa fedha 2018/19 kwa kukusanya zaidi ya asilimia 20 ya makisio yake.

## 4.0 Utekelezaji wa Matumizi Mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani katika MSM

OR-TAMISEMI kupitia Idara ya TEHAMA (DICT) imeendelea kuboresha zaidi Mfumo wa LGRCIS kwa kuunganisha na Mifumo mingine ya TEHAMA ikiwemo IFMIS, GePG, GIS, GoTHOMIS na FFARS. Mfumo wa LGRCIS kwa sasa unaweza kutuma takwimu za mapato kwenda IFMS na kwenye Ubao wa mapato (*Revenue Dashboard*).

Napenda kuchukua fursa hii kusisitiza Wakurugenzi wote kuhakikisha takwimu zote za mapato katika mfumo wa LGRCIS zinafanyiwa usuluhisho na kutumwa katika mfumo wa IFMS (Epicor) kwani taarifa zote za Mapato na Matumizi ya fedha zinatakiwa kutolewa kupitia mfumo huo. Aidha takwimu za ukusanyaji zinazosomwa leo ni kwa mjibu wa taarifa zilizofanyiwa usuluhisho na kutumwa katika mfumo wa IFMS (Epicor).

## 5.0 Changamoto za ukusanyaji mapato ya ndani.

Baadhi ya changamoto zilizozikabili Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani katika kipindi cha Julai - Desemba katika mwaka wa fedha 2018/19 ni pamoja na:-

i) Baadhi ya wanunuzi kuchelewa kulipa ushuru kwa Halmashauri na kepelekea Halmashauri hizo kuonekana zimekusanya chini ya kiwango;
ii) Baadhi ya Halmashauri kutegemea zaidi chanzo kimoja ambapo kushindwa kukusanya kutoka kwenye chanzo hicho kunaweza kupelekea Halmashauri hizo kushindwa kujiendesha;

iii) Matumizi mabovu ya mifumo ya kukusanyia mapato kwa njia za kielekroniki kwa baadhi ya Halmashauri;
iv) Baadhi ya Halmashauri kutumia takwimu za makisio zisizo na uhalisia;
v) Kushindwa kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vipya vinavyobuniwa na Halmashauri;
vi) Baadhi ya Halmashauri kutokua na Sheria ndogo za mapato;
vii) Uandaaji wa taarifa za mapato na matumizi ya mapato ya ndani usio wa kuridhisha hasa kupitia Mifumo ya kielektroniki mfano, Epicor.

## 6.0 Mikakati ya kutatua changamoto

i) OR-TAMISEMI imeendelea kuzisimamia kwa karibu Halmashauri zote zinazoonesha kusuasua katika suala la ukusanyaji wa mapato. Baadhi ya hatua ni kuwachukulia hatua za kinidhamu Wakurugenzi wote watakaodhibitika kutokusimamia vyema suala la kukusanya mapato ya ndani.
ii) Mikoa na Halmashauri zinapaswa kuendelea kusimamia utoaji wa taarifa kupitia Mifumo ya kielektroniki ikiwemo kazi za usuluhishi na kusafisha takwimu chafu kwenye mfumo wa Epicor 10.2 ili kuwezesha kuwa na takwimu sahihi kwenye *Dashboard* ya mapato ya ndani na kwa wakati.
iii) OR-TAMISEMI imeandaa Mwongozo wa ukusanyaji mapato ya ndani *(Revenue Manual)* ili kuzisaidia Halmashauri kuwa na uelewa wa pamoja kwa watu wote juu ya masuala ya ukusanyaji wa mapato kuanzia suala la kupanga, kukadiria, kukusanya, kutumia, ukaguzi wa nje na ndani na kutoa taarifa.
iv) OR-TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wadau wengine wengi katika kuhakikisha Halmashauri zinakusanya ipasanyo mapato ya ndani. Wadau hao ni pamoja na Wizara za Kisekta, Wizara ya Fedha na Mipango, Wadau wa Maendeleo, Watu binafsi, Mashirika mbalimbali na Sekta zingine zinazojihusisha na Halmashauri Nchini.
v) OR-TAMISEMI ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290,

amapo Sheria hiyo imetumika kwa muda mrefu tangu 1982 hivyo, marekebisho hayo yanalenga kuweka uhalisia wa utendaji wa sasa katika namna bora zaidi ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 7.0 Hitimisho

Tunapenda kuzipongeza Halmashauri zote zilizofanya vizuri katika kukusanya mapato ya ndani kwa kipindi hiki cha nusu mwaka na tunazitaka Halmashauri hizo na ikiwezekana Halmashauri zote ziendelee kuongeza bidii ili kuweza kufikia malengo ya mwaka ili kuweza kuendelea kutoa huduma bora kwa Wananchi.

Aidha, kwa zile Halmashauri 21 zilizokusanya chini ya asilimia 20, nawaagiza Wakuu wa Mikoa kujitathmini na kuwasilisha maelezo OR-TAMISEMI ya sababu za kushindwa kufikia malengo ya makisio na mikakati gani waliyojiwekea kuhakikisha wanafikia malengo ifikapo Juni, 2018.

Naenedelea kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo yetu ya Ukusanyaji wa Mapato na Utoaji wa Taarifa kwa kutumia Mifumo ya kielektroniki ili kuepuka ufujaji wa Fedha za Umma na udanganyifu usiokuwa wa lazima kutokana na Watumishi wa Halmashauri wasiokuwa waaminifu.

Taarifa hizi ni kwa mujibu wa takwimu zinazoonekana kwenye *Revenue Dashboard* kama tulivyooelekeza kipindi cha nyuma kuwa sasa taarifa hizi zitakua zinatolewa kwa mujibu wa Mifumo ya kielektroniki hasa Epicor ambao unapeleka moja kwa moja kwenye *Dashboard* ya mapato. Aidha, imebainika kuwepo kwa uzembe wa baadhi ya Waweka Hazina kushindwa kusimamia uingizwaji wa takwimu za mapato ya ndani kwenye Mfumo wa Epicor. Suala hili haliwezi kuvimilika na Waweka Hazina hao watapaswa kujitathmini na kutoa maelezo OR-TAMISEMI.